



TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwa kushirikiana na Taasisi ya Afya ya UKIMWI ya AMREF kupitia Mradi wa AFYA KAMILIFU unaofadhiliwa na CDC, ambao unafanya kazi na mkoa wa Tanga kitengo cha VVU/ UKIMWI na TB / VVU unatangaza nafasi zifuatazo:-

1. Tabibu daraja II (2)

Eneo la kazi: Hospitali Teule Wilaya Kilindi(01), Kituo cha afya Kwediboma (01)

MAJUKUMU

- Kutoa huduma za kinga na Tiba.
- Kutambua na kutibu magonjwa
- Kutoa huduma ya Afya ya Msingi
- Kutunza takwimu zinazohusiana na kazi.
- Kuwaanzishiwa dawa wateja wapya waliogundulika na maambukizi
- Kutunza Siri za wagonjwa

VIGEZO VYA MWOMBAJI

- Awe Tayari kufanya kazi wilaya husika (Kilindi)
- Astashahada/Stashahada katika tabibu katika vyuo vinavyotambulika na Serikali.
- Uzoefu wa miaka 1 - 3 katika kazi ya utabibu

UJUZI NA UWEZO

- Uwezo kumaliza kazi kwa wakati uliopangwa
- Kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea na kuchukua hatua kwa wakati
- Kuwa na uwezo wa kutoa ushauri kwa jamii juu ya masuala ya kiafya
- Uwezo wa kutumia compyuta ni sifa ya ziada

2. Mtoa Huduma za VVU na UKIMWI Ngazi ya Kituo/Jamii (Facility Based CIW) Nafasi (04)

Eneo la kazi: Zahanati ya Kwinji (01), Kituo cha Afya Kwediboma (01), Hospitali Teule(01) Zahanati ya Kibirashi (01)

MAJUKUMU YA JUMLA:

Kutoa huduma za VVU na UKIMWI ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa lengo la kuibua wateja wapya, Kuunganisha wateja wapya kwenye huduma za Kinga, matibabu na matunzo. Ufutiliaji wa upatikanaji huduma kwa wateja na ushauri nasaha kuhusu ufuasi endelevu wa dawa na vipimo husika hususan upimaji wa kiwango cha VVU kwa wateja wanaotumia ARV.

MAJUKUMU/KAZI MAHUSUSI:

- Ujazaji bora wa nyenzo za ufuutiliaji wateja wanaohuduria klinik (Appointment register) na mifumo wa kielekronic wa utunzaji takwimu (database) ili kubaini wateja wasiohuduria kliniki kwa wakati (MISAP) au wanaopotea (LTFU)
- Kutumia taarifa za mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za wateja ili kutambua na kuchambua majalada ya wateja waliopotea (MISAP/LTFU)
- Kufuatilia, kutafuta wateja wanaopotea kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na simu au ufuutiliaji wa wateja nyumbani.
- Kurekodi na kutoa taarifa ya matokeo ya ufuutiliaji wa wateja .
- Ufuutiliaji wa wateja (watoto na wenyе umri barehe) katika vitengo mbalimbali vya huduma na matunzo na kurudisha kwenye huduma wanaopotea .
- Kutoa huduma za rufaa za ndani na nje ya kituo ili kuwezesha upatikanaji wa huduma endelevu
- Ufuutiliaji na utoaji wa taarifa za viso vitokanavyo na VVU na UKIMWI
- Kutoa elimu kuhusu VVU na UKIMWI, kufanya uchunguzi wa awali kwa lengo la kutambua watu wenyе sifa za kupimwa VVU (Screening for eligibility criteria for HTS) kwa wagonjwa wanaohuduria katika kituo cha matibabu.

SIFA ZA MUOMBAJI

- Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi
- Awe na Cheti cha mafunzo ya Utoaji Huduma za Afya ngazi ya Jamii (Certificate of Community Based Health Services) au ngazi nyinginezo zinazohusiana kutoka chuo kinachotambulika kitaifa.
- Wenyе mafunzo ya ziada kuhusiana na utoaji wa huduma za afya/VVU na UKIMWI watapewa kipaumbele.
- Awe na uwezo na uzoefu wa Kutoa ushauri nasaha na kupima VVU, utoaji wa huduma za matibabu ya ARV pamoja ufuutiliaji wa wateja kuhusiana na ufuasi wa dawa na vipimo husika ikiwa ni pamoja na utafutaji wa wateja wanaopotea.
- Uwezo wa kutunza siri za wateja/wagonjwa na taarifa zote zilizopo katika mifumo ya taarifa za wateja/wagonjwa.
- Uwezo wa kutoa huduma kwa watu wote bila unyanyapaa au ubaguzi
- Awe mtu mwenye kukubalika na watu kwenye ngazi ya kituo na jamii



3. MTEKNOLOJIA DAWA DARA LA II

Eneo la kazi: Kituo cha Afya Songe

Sifa za kuingilia kazini

Stashahada katika fani ya Uteknolojia kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

Majukumu/ kazi mahususi

- Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
- Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
- Kuchanganya dawa
- Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
- Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
- Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
- Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa
- Kusaidiana na Mfamasia wa Wilaya kutekeleza majukumu yanayohusianana taaluma yako.

Kila muombaji aliyetimiza vigezo anahimizwa kuomba kwa kuambatanisha CV, Nakala ya vyeti na barua ya maombi kwenda **Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) S.L.P 18 KILINDI** mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 14/09/2021**

Gracian M. Makota

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KILINDI**

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KILINDI*